**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA**

**MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI**

**711** **KISWAHILI**

**Muda: Masaa 3** **Ijumaa, 04th May 2012 Asubuhi**

---

**Instructions.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali kumi na sit (16).
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali mawili kutoka kila sehem **B** na **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** Zina jumla ya alama **sitini (60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha majibu.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama 4.

1. (a) Fafanua maana ya nomino za pekee.
   (b) Taja mifano miwili ya nomino za pekee na tunga sentensi kwa mojawapo.

2. (a) Eleza maana ya kitenzi kauli ya kupeswa.
   (b) Tunga sentensi moja inayoonyesha matumizi ya kauli ya kupeswa.

3. Toa tofauti kati ya sentensi ya sharti na sentensi ya maelezo kwa kutoa maana na mfano wa kila moja.

4. (a) Eleza maana ya vitenzi vya nje.
   (b) Taja vitenzi viwili vya nje na tunga sentensi moja kwa kimoja.

5. Eleza maana ya viambishi vya wakati kisha taja viambishi viwili vya wakati na toa sentensi za matumizi.

6. Fafanua maana ya kishazi tegemezi kwa kutoa sifa zake mbili na mfano mmoja wa sentensi.

7. (a) Taja ngeli mbili za nomino zinazohusisha viumbe hai.
   (b) Eleza sifa moja ya kila ngeli uliyotaja.

8. (a) Toa maana ya tamathali ya usemi.
   (b) Taja tamathali mbili na eleza matumizi yake katika kazi ya fasihi.

9. Eleza umuhimu wa matumizi ya lugha ya picha katika ushairi wa Kiswahili kwa hoja mbili na mifano.

10. Taja mitindo miwili ya usimulizi katika kazi za fasihi simulizi na eleza kila mmoja.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili kutoka sehemu hii. Kila swali kina alama 15.

11. Eleza kwa hoja sita umuhimu wa kutumia Kiswahili sanifu katika vyombo vya habari nchini Tanzania.

12. Fafanua kwa hoja sita matatizo yanayowakumba wanafunzi wa sekondari katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

13. Kwa hoja sita, eleza mchango wa wanafasihi wa Kiswahili katika kukuza lugha na utamaduni wa Mtanzania.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU C (Alama 30)

Soma kifungu kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:

Katika kijiji cha Mlembule, wazee walikuwa wakiheshimika na kusikilizwa. Kauli yao ilikuwa kama amri na walitoa ushauri kwa busara. Lakini hali imebadilika kwa kasi kubwa. Vijana wameanza kuona wazee kama watu wa kale wasiokuwa na mchango katika maisha ya sasa. Wanavikwepa vikao vya ukoo na kushindwa kuzingatia maadili ya jamii. Lugha wanayotumia imeharibika na siyo ya staha. Jamii imeanza kushuhudia ongezeko la migogoro ya kifamilia, uhalifu na ukosefu wa heshima. Hii imewafanya baadhi ya wazee kukata tamaa na kukosa hamu ya kushiriki katika maisha ya kijamii.

14. (a) Eleza maudhui matatu yaliyopo katika kifungu.
    (b) Taja sababu mbili zinazochangia hali ilivyojitokeza katika jamii ya Mlembule.

15. Kwa hoja sita, eleza namna jamii ya sasa inavyoweza kufaidika kwa kuyarejea maadili ya Kiafrika.

16. Jadili kwa hoja sita nafasi ya lugha ya Kiswahili katika kujenga maelewano na mshikamano katika jamii za Kitanzania.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org